

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

HALMASHAURI YA MANISPAA DODOMA

(Barua zote zipelekwe kwa Mkurugenzi wa manispaa)

MKOA WA DODOMA

Simu:

2324817/2321550

Fax: 2324817/2321550



OFISI YA MKURGENZI WA MANISPAA,
S.L.P. 1249

Dodoma

E-mail:

Unapojibu tafadhali taja:
HMD/MLF/M.60/3/23

06/06/2017.

YAH: ZUIO LA BIASHARA YA NGURUWE NA MAZAO YAKE KUTOKANA NA KUZUKA KWA UGONJWA WA HOMA YA NGURUWE WILAYANI DODOMA MJINI

Kwa mamlaka niliyopewa na Kifungu cha ~~17~~ cha sheria ya magonjwa ya Mifugo Namba 17 ya Mwaka 2003.

Mimi **Dr. Innocent Peter Kimweri (BVM)**, Daktari wa Mifugo Wilaya ya Dodoma Mjini, natangaza rasmi kwamba Wilaya ya Dodoma Mjini inamlipuko wa ugonjwa wa Homa ya Nguruwe na kwa sasa **NAWEKA ZUIO LA BIASHARA YA NGURUWE NA MAZAO YAKE HADI HAPO ITAKAPOTANGAZWA VINGINEVYO.**

Hakuna mnyama yeyote jamii ya Nguruwe (Ngiri, nguruwe pori au Nguruwe wa Kufugwa) ataruhusiwa kuingia, au kutoka nje ya eneo la Wilaya ya Dodoma pasipokuwa na ruhusa ya maandishi kutoka kwa Daktari wa Mifugo wa Wilaya ya Dodoma.

Hakuna bidhaa inayo tokana na Nguruwe, ikiwemo mbolea, kinyesi, mkojo na damu kitakacho ruhusiwa kuingia au kutoka nje ya Wilaya ya Dodoma pasipokuwa na ruhusa ya maandishi kutoka kwa Daktari wa Mifugo wa Wilaya ya Dodoma mjini.

Aidha hakuna mnyama yeyote wa jamii iliyotajwa hapo juu kwenye aya 3 atakaye kusanywa kwa ajili ya biashara pasipokuwa na ruhusa ya maandishi kutoka kwa Daktari wa Mifugo wa Wilaya ya Dodoma.

Uchinjaji wa nguruwe ndani ya Wilaya husika, utafanyika chini ya usimamizi madhubuti wa mtaalamu wa afya za mifugo mwenye dhamana.

.....
(Dr. Innocent Peter Kimweri)

Nakala

- 1) Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo
Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi
S.L.P. 9152.
DAR- ES-SALAAM.
- 2) Afisa Mfawidhi
Kituo cha Uchunguzi wa Magonjwa ya Mifugo
S.L.P. 1752.
DODOMA.
- 3) Katibu Tawala Mkoa
S.L.P. 914
DODOMA.
- 4) Mkuu wa Wilaya
S.L.P. 105
DODOMA.
- 5) Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya
S.L.P 1249
DODOMA.
- 6) Mhe. Hakimu wa Wilaya
S.L.P...
DODOMA.
- 7) Mkuu wa Polisi (W)
S.L.P 912
DODOMA.
- 8) Watendaji Kata Halmashauri ya Manispaa
DODOMA
- 9) Maafisa Afya na Maafisa Mifugo
Halmashauri ya Manispaa Dodoma.
- 10) Mbao za matangazo.